Mtoto mwenye miaka 10, kibibi Juma, mwanae halima hamis amepotea toka, Desemba 4 huko Kibokoni akiwa amevalia rinda jekunde lenye madda meupe. Anazumgumza Kiswahili Habari zo-zote kuhusu alipo ripelekwe Central Police Station

Mchungwe Mwanetu

MCHUNGUE msichana - ukimwona anaanza kuwaonea haya wavulana na kukwepa kuchaganyika nao kama alivyokua miezi ama miaka ya nyuma, jua yuko katika daraja la kutafuta mchumba!

Na ukimwona msichana anaanza kuchungua maisha ya wavulana na bado anaogopa kuchaganyikana nao, jua huwa amekwisha pata mchumba!

Na baadaye ukija ukamkuta anachanganyikana na wavulana ikiwa lazima, fahamu huwa amekwisha-kuwa na watoto!

Na hatimaye ukimwona anapenda kuchanganyikana na wavulana lakini sasa wavulana wanamkwepa, jua wazi huwa ameshajukuu yaani amekuwa nyanya!

Leonard Bob Rubia, MALAVA.

WAKIHUDHURIA tamasha iliyoandaliwa na balozi wa Omani katika Hilton Hotel kuadhimisha siku ya Taifa la Omani ni (kutoka kushoto) mfanyibiashara Mombasa Bw. Mohamed Dooh, Mbunge said Hemed, Bw. A. M. Rahim wa Nairobi, John Vespa kutoka Mombasa, Bi. Amina Johnson na Mhe. Sheriff Nassir Mbunge na pia waziri mdogo wa Kazi.

MZEE Kombo akipokea hundi ya Shs. 6,000 alipostaafu baada ya kuitimikia kampuni ya Rentokil kwa mda wa miaka 16. Kushoto ni Meneja Robin Mvunguh akishuhudia sherehe hiyo.

WATOTO viziwi wa shule ya Kwale wakiadaliwa mapocho pocho na wawake wa Lions Club ya Mombasa kati kwenya tafrija iliyoandaliwa na kina mama hao.

Tujumuike Na Rais Moi Kujenga Kenya Yetu 1983

TUNAHITAJIKA KUZINGATIA KWA makini agizo la Mtukufu Rais Moi kuhusiana na uchumi wa nchi; zingatio ambalo Rais wetu amewaomba viongozi wawafahamish wananchi na kuwaeleza kwa makini kuhusu matatizo tunayoweza kukanili siku zijazo. Rais wetu anafanya kila liwezakanalo kuona maisha ya wananchi wa Kenya yanakuwa ya kuridhisha.

Lazima tukubali kwamba Ulimwengu mzima umekumbwa na matatizo ya kila aina hasa kwa karne hii tuliyonayo, lakini nchi yetu ina afadhali kuliko nchi nyingi hasa tukiangalia tulio karibu nao. Ingawa tungali tunajivuna na kuona tuko katika hali ya kuridhisha, tunahitajika tukaze mikanda yetu tuone tumeweza kukubiliana na shida na matatizo yatakayoweza kutufikia.

Kila mwananchi wa Kenya ana wajibu wa kufahamu kuwa nchi yetu ina afadhali sana ukilinganisha na wenzetu ambao wameshapambana na matatizo makubwa; matatizo ambayo yamewafanya wananchi wapate taaby ya kila aina. Ni juu yetu kutekeleza kwa vitendo mawazo ya busara tunayotolewa na Rais Moi pamojana viongozi kuhusu jambo hilo.

Tukiwa langoni kuuaga mwaka wa 1982 na kuukaribisha mwaka mpya wa 1983, tunahitajika kufahamu kuwa lazima tufanye bidii katika kila jambo ili tuendelee kushi kwa furaha na amani. Matokeo ya Agosti 1 mwaka huu ni jambo ambalo lazima tuliepuke kwani limeleta vifo vingi vya wananchi ambao hawakuwa na hatia; jambo ambalo limewahi kufanyika nchi nyingine na kuleta maovu yaliyoharibu kabisa uchumi wa nchi hizo.

Rais wetu kila wakati anatusisitiza tuishi kwa amani sababu wananchi wa Kenya wote ni ndugu na umefika wakati kila Mkenya ajitambulishw kama Mkenya badala ya kujiona yeye ni kabila fulani, dini fulani ama rangi fulani. Tujumuike pamoja, tushikane mikono na kufanya kazi kwa juhudi zetu zote kupambana na kila linaloweza kutufikia. Lazima uthabiti wa nchi yetu uzidi kutiwa maanani; uthabiti ambao unatupa wananchi wa nchi hii demokrasia ya kila aina.

Wakenya tuna uwezo wa kuwachagua viongozi tunaowataka, kujifanyia mambo yetu ya kuinua hali zetu za maisha kwa njia za kihalali na hata tuna uwezo na uhuru wa kuabudu dini zetu, jambo ambalo nchi nyingi zimeshindwa kutekeleza. Na yote hayo tumeyapata kutokana na uthabiti ulioko nchini toka Hayati Mzee Jomo Kenyatta alipokuwa Rais wetu na hadi wakati huu ambapo Mtukufu Rais Moi ndiye anashikilia usukani.

Namaliza kwa kuwaomba Wakenya wenzangu tuwe tukifuata kwa vitendo na kwa dhati ya mioyo yetu maongozi ya busara ya Baba Wetu wa Taifa, Mtukufu Rais Daniel arap Moi ili tuufanye mwaka wa 1983 uwe wamafanikio na maendeleo ya kutosha na tuepukane na vitendo vyovyote vinavyoweza kuvuruga uthabiti wa nchi yetu.

Abdulrahman Sheriff

Washindi Wengine Ya Maendeleo Ya Wanawake

WASHINDI wengine wanaendelekupokea zawadi zao katika mashinda ya Maendeleo Ya Wanawake yaliodhaminiwa na Coastal Bottlers. Juu wanaoneka Mbwana Suleman Mwaringa wa Majengo na Israel Komora wa Bamburi wakipokea zawadi za saa. Chini Bi. Mwajuma Abdalla wa Kisauni amejishindia jiko la spaki. Zawadi zote hizo zilikabidhiwa wa shindi na Meneja wa Coastal Bottlers Bw. Mohammed Qoyyan.

PICHA: NATIONAL STUDIO

HARUSI YA WANASOKA

HARUSI ya kukata na shoka inatarajiwa kufanyika baina ya Katibu Mkuu wa Black Panther FC Ali Mbarak Ali na mwanae Shariff Abdillahi Omar Bin Agil mwishoni mwa wiki hii.

Akitangaza ratiba ya sherehe na shamrashamra za harusi hiyo, mwenyekiti wa Black Panther, Omar Sheriff Maulana alisema leo Ijumaa kutakuwako na kesha katika uwanja wa Mwenbe Tanganyika ambapo mwimbaji wa taarab atatumbuiza wageni.

Maulana aliyeandamana na Mwenyekiti wa Bahia Stars FC, Ali Awadh alisema kuwa kesho Jumamosi, Akdi-Nikah itafanyika kwenye msikiti wa Al-Azhar baada ya swala ya Isha.

Mwenyekiti huyo aliviomba vilabu vyote vihudhurie kwenye sherehe hizo na akasema watu kadha mashuhuri wamealikwa.

ALI MBARAK ALI

Ngoma na shamrashamra zinatarajia kusikika mtaani hapo wakati vijana wa Panther na Bahia watakapokuwa wakisherehekea harusi ya Mwandishi wao.

Babake Bibi Arusi, Shariff Abdillahi alikuwa mchezaji maarufu wa Mwenye, ambayo hapu rali ilikuwa ikijulikana kama Liverpool.

JISHINDIE

MIAVULI AU T-SHIRT MARIDADI KATIKA SHINDANO JIPYA LA KUJAZA MANENO

KWENDA KULIA:

1. United Kingdom
3. Moyo
8. Sehemu ya mnyama
10. Nchi Arabuni
11. Langalie
12. Mahali penye maji mengi baharini
13. Nguvu za Mungu
18. Wazimu
21. Hutengeza bara bara
23. Uadilifu
24. Natasi, sehemu ya ardhi
25. Zuia vita
26. Atatunga ndoa
27. Tamko la kukataa.
19. Kiungo cha maneno
20. Azidi kimo
21. Tunza mtoto
22. Ota, chipuza.

KWENDA CHINI:

1. Ukoa haigeuki
2. Mtoto wa ndege
4. Uchatu
5. Sikukuu ya Kiislamu
6. Silaha za kutatumia
7. Sikwamba hana
8. Mwiko zaidi ya mmoja
9. Aeu kama ilivyo
14. Bembeleza
15. Shirika, Mkao
16. Wenyeji wa nchi
17. Taka kitu kimombo
18. Cha kujiangalia

Washindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 152

1. Ali Bakari Sanduku La Posta 86922 Mombasa.
2. P. W. Mpwipniro Sanduku la Posta 90404 Mombasa.
3. Jimmie Munene Sanduku La Posta 87310 Mombasa.

Washindi waombwa wafike afisini mwa COASTWEEK.

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO 152 —

KWENDA KULIA:

1. KUNGU, 6. KAZA, 7. NAAM, 10. ADAI, 11. ANAO, 12. SH, 13. BA, 14. HIMU, 16. TAIB, 18. JA, 19. OA, 20. TUMA, 23. BOSS, 25. AZOA, 26. ISHA, 27. UBALE.

KWENDA CHINI:

1. KADHI, 2. UZA, 3. NAIBU, 4. UNA, 5. KAA, 6. KASHATA, 8. ANGA, 9. MOMBASA, 15. MUMO, 16. TABIA, 17. IOSHE, 21. UZI, 22. AAU, 24. OSI.



SWAHILI CROSSWORD NO 153

JINA ....

SANDUKU LA POSTA ....

....

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malamiko yoyote yatakayokubaliwa. Washindi watatu kila baada yawiki mbili watapata miavuli au T-Shirt maridadi. Shindano hili limeshaminiwa na *COASTWEEK* Limited Mombasa.,
Jawabu za Fimbo hili lipelekwe kwa: *Muhariri COASTWEEK, Sanduku La Posta 87270 Mombasa, Kenya.*
Siku ya Jumatano tarehe December 29, 1982, saa nne asubuhi shindano hili litakuwa mwisho.